

## Migogoro yaiteza wizara ya mifugo

Mussa Juma, Mwananchi  
mjuma@mwanchi.co.tz

Manyara, Wizara ya maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imejipanga kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini, kwa kuongeza maeneo ya nyanda za malisho ya mifugo.

Wakati ikipanga kwa hilo, kumeibuka tena mapigano ya wakulima na wafugaji wilayani Kiteto mkoani Manyara katika eneo la hifadhi ya Emborey Murtangos.

Imeelezwa mpaka sasa watu kadhaa wameuawa, wengine kujeruhwa na mali kadhaa kuharibiwa.

Mapigano hayo yamekuwa yakinoteka baada ya wafugaji kudaiwa kuingiza mifugo katika mashamba au wakulima kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa malisho ya mifugo.

**"Malisho ya mifugo ni changamoto kubwa kutokaka na Idadi ya mifugo kuongezeka nchini lakini pia kuna mabadiliko ya tabla nchi ambayo yamepunguza mallsho."**

Profesa Nonga

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo katika wizara hiyo, Profesa Hezron Nonga amesema wizara hiyo imejipanga kukomesha mapigano hayo kwa kuanzia na kutatua changamoto ya malisho ya mifugo.

Profesa Nonga alisema kwa sasa wizara kwa kushirikiana na halmashauri wanaendelea kutenga maeneo ya nyanda za malisho na pia, imeanza kusambaza mbegu za malisho ya mifugo kwa kushirikiana na wadau wengine.

"Tunataka kila mfugaji awe na eneo la uhakika wa malisho yake na hapa ndiyo sababu sasa tunataka wafugaji kuwa na mifugo michache yenye tija," alisema.

Profesa Nonga alisema kama wafugaji wakifuga kisasa na kuwa na uhakika wa malisho hakutakuwa na migogoro na wakulima.

"Lakini pia tunataka wakulima na wafugaji waheshimiane na kuthaminiana kwani kila mmoja kuna sehemu anamtegemea mwengine," alisema.

Alisema miradi hiyo ambayo imeanzishwa katika maeneo ya wilaya za Monduli, Longido, Simanjiro itasaidia sana kukabiliana na uhaba wa malisho ya mifugo na hivyo kupunguza migogoro.

Mratibu wa programu ya miradi midogo ya mazingira katika mfuko wa GEF, Faus-tine Ninga alisema mashirika 24 yalipati-wa ruzuku yenye thamani ya Shs1.5 bilioni kutekeleza miradi ya mazingira ili kusaidia jamii hizo.

ma,  
aki-  
sini  
  
lani  
na  
ise-  
  
sho  
ito-  
na-  
jaa  
idhi  
jine  
mu  
  
iae-  
iwa  
ian-  
ndo  
laji-  
isha  
  
pali,  
ido-  
gine  
o na  
cuji-  
ema

## MOROGORO>> Miongoni mwa

**UHURU**

MAONI YA MHARINI

H

### Mikakati kukomesha wizi wa mifugo, vurugu jamii za wafugaji iwe endelevu

SERIKALI katika Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, imelaani vikali vitendo vinavyofanywa na baadhi ya jamii za wafugaji vya kuiba mifugo, hali inayosababisha uvunjfu wa amani katika wilaya hiyo.

Akizungumzia kadhia hiyo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alisema miongoni mwa wafugaji wamekuwa wakiwalibia wenzao ng'ombe na kusababisha migogoro.

Kwa sababu hiyo, Shaka alionya hatakulali vitendo hivyo viendelee Kilosa kwa kuwa ni albu na vinachochea uvunjfu wa amani na kuzitaka jamii za wafugaji kuishi kwa maelewano na yoyote atakayebainika ndiye kikwazo atashugulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Tunaunga mkono hatua ya mkuu huyo wa wilaya kukemea wizi wa mifugo na tunawakumbusha wakuu wote wa wilaya zenyé jamii kubwa za wafugaji na wakulima nao kusimama mstari wa mbele katika kukomesha vitendo hivyo.

Baadhi ya mikoa yenyé wilaya zenyé jamii kubwa hususan Manyara, Arusha, Dodoma, Mara na Morogoro mara kadhaa ziliwahi kuingia katika machafuko yaliyosababishwa na wakulima kupigana na wafugaji, hivyo wakati umefika kwa wakuu wa wilaya husika kukomesha matukio hayo yenyé kuhatarisha uvunjfu wa amani.

Tunasisitiza juhudzi zilizoanza kuchukuliwa na Shaka, ziungwe mkono kwa kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinachunguza na kuwachukulia hatua kali za kisheria wote wanaopanga njama hizo.

Ni dhahiri vyombo vya dola vikishirikiana na viongozi wa vijiji, kata na tarafa zote zenyé migogoro inayotokana na wizi wa ng'ombe au wafugaji kulisha mifugo katika maeneo ya wakulima, itasaidia kukomesha kila uhalifu na kuleta amani.

Athari kubwa zinazobaki baada ya vitendo vya wizi au wafugaji kuvamia mazao ya wakulima, ni miongoni mwa wananchi kupoteza maisha au kujeruhiwa kutokana na mapigano yanayoibuka kila mara chanzo chake kikiwa wizi huo wa mifugo au uvamizi katika maeneo ya wakulima.

Tunawashauri viongozi wa vijiji vinavyokumbwa na machafuko yanatokana na wafugaji au wakulima kuwa wa kwanza kuvitaarifu vyombo vya dola mapema katika kuhakikisha mitandao yote ya uhalifu au inayopenda machafuko inadhibitiwa kabla kuleta madhara.

Aidha, tunaa mini miongoni mwa hatua za kukomesha vitendo hivyo ni viongozi wa vijiji kuchunguza na kuyataja kwa vyombo vya dola majina ya watu wanaotuhumiwa kuhusika na uhalifu huo, kwani wakitiwa mbaroni na kufikishwa mahakamani amani na utulivu itabaki kuwa endelevu katika jamii nyingi za wafugaji na wakulima.

Pia, wakati umefika kwa vyombo vya dola kupanga mikakati endelevu ya kudhibiti wizi na uvamizi wa mashamba ya wakulima unaofanywa na wafugaji kwa lengo la kustawisha amani iliyopo.

Uje  
ma  
ur  
m  
shug  
zini  
kish

